

A black and white line drawing of a person wearing a headwrap and a long tunic, standing in a field. They are holding a long wooden tool and appear to be working on a raised garden bed made of vertical logs. The background shows more of the agricultural landscape with trees and hills.

NAWEZAJE KUTHIBITISHWA KWA AJILI YA
UFUGAJI NYUKI NA MAZAO YA PORINI




1 Je, ninahitaji kujua nini kuhusu uthibitisho wa Mazao ya Porini na Ufugaji Nyuki?

Shughuli za Ukusanyaji wa Mazao ya Porini na Ufugaji Nyuki zinaweza kuthibitishwa kulingana na viwango vya kilimo-hai vilivyopo. Shughuli hizi zifanyike kulingana na viwango na kuthibitishwa na mamlaka ya uthibitisho.



Shughuli za ukusanyaji wa mazao pori na ufugaji nyuki zinapaswa kufanywa bila ya kuharibu mazingira na zisitumie viambato ambavyo si vya asilia kama vile kemikali zisizoruhusiwa.




2

Ni vitu gani vinathibitishwa katika Ukusanya wa Mazao ya Porini?

Mazao yanayoota porini na mali ghafi zinazotoka porini: ikiwemo maeneo ya kukusanyia na shughuli nyingine zozote zinazofanyika baada ya ukusanyaji.

Mifano ya mazao ya porini:



Uthibitisho pia utahusisha wabia wote wanaoshughulika na ukusanyaji wa mazao pori:

- Wamiliki wa ardhi au mameneja
- Wakusanyaji mazao au wakala wa maeneo
- Wasindikaji
- Anayeendesha mashine za kusindika mazao pori


Wabia hawa wapewe mikataba na kutaarifiwa kuhusu sharia za ukusanyaji mazao pori

3

Ninahitaji nini ili niweze kuthibitishwa kwa Ukusanyaji wa Mazao Pori?

Shughuli za ukusanyaji wa mazao pori zifanyike kulingana na viwango vya kilimo-hai.

Shughuli hizi zinajumuisha:



Ainisha na weka mipaka maeneo ya ukusanyaji wa mazao pori. Mazao yasikusanywe kutoka maeneo ambayo kemikali zisizoruhusiwa zinatumika



Toa mafunzo kwa wakusanyaji wote kuhusu mbinu bora za ukusanyaji



Usutumie mbiriu za ukusanyaji ambazo huhanibu mazingira



Weka kumbukumbu ya mazao yaliyokusanya

Angalizo: Epuka kukusanya mazao kutoka maeneo ya hifadhi au spishi zilizokatazwa

4

Ni vitu gani vinathibitishwa katika Ufugaji Nyuki?

Mazao ya nyuki yanayotokana na shughuli za ufugaji nyuki shambani.

Kwa mfano:



Uthibitisho utahusisha maeneo yafuatayo:

- Vyanzo vya makundi ya nyuki na nta
- Maeneo wanapokula nyuki, mizinga na ufugaji
- Kuvuna mazao ya nyuki na hifadhi yao
- Kusindika mazao ya nyuki
- Kumbukumbu za ufugaji nyuki
- Mmiliki na wafugaji wengine shambani

Kwa habari zaidi kuhusu ufugaji nyuki kwa vijwango vya kilimo-hai na uthibitisho, wasiliana na Shirika la Taifa la Kukuza na Kuendeleza Kilimo-hai (NOAM) katika nchi yako.

5

Nawezaje kuthibitishwa?

Wakusanyaji wa mazao pori na wafugaji wa nyuki wanaweza kutafuta uthibitisho kuititia hatua zifuatazo.

Katika Mwaka wa Kwanza:



Hatua 1: Soma habari kuhusu viwango na habari mzingine kutoka Shirika lako la Taifa la Kilimo-hali.

Hatua 2: Ulizia habari kutoka katika Mamlaka za Uthibitisho zilizopo. Wasiliana na Mamlaka na upate habari husika kuhusu viwango, mchakato wa maombi, gharama za uthibitisho, na taratibu.

Hatua 3: Chagua Mamlaka ya Uthibitisho inayofaa. Jaza na wasilisha maombi, jadiliana nao gharama za uthibitisho, taratibu na malipo ya ada. Weka saini mkataba wa ukaguzi na uthibitisho na Mamlaka hiyo.



Hatua 4: Ukaguzi. Panga na Mamlaka ya Uthibitisho lini mkaguzi atakuja kukagua shughuli za ukusanyaji wa mazao pori na ufugaji nyuki na kumbukumbu. Mtu mmoja atafuatana na kumsaldia mkaguzi wakati wote.



Hatua 5: Jadili ripoti ya ukaguzi na Mkaguzi. Soma ripoti kwa uangallfu na kagua iwapo ina makosa yoyote au haloleweki.



Hatua 6: libu maswali yote kutoka kwa mkaguzi. Kagua na timiza masharti yote yanayohitajika kwa ajili ya uthibitisho wako.

Hatua 7: Uamuzi wa uthibitisho. Mamlaka ya uthibitisho hatimaye itakutaarifu matokco ya ukaguzi na uamuzi wa uthibitisho.

6


Nawezaje kuendeleza uthibitisho wangu?

Shughuli za ukusanyaji wa mazao pori na ufgajji nyuki zitakaguliwa kila mwaka na Mamlaka ya Uthibitisho. Hahakikish masharti yote ya uthibitisho kutoka kwenye Mamlaka ya Uthibitisho yanatimizwa.

Kwa hiyo, unapaswa kufanya yafuatayo:



Fanya marekebisho yaliyoagizwa, wakati viwango vikibadilishwa



Weka kumbukumbu zako vizuri ziwe na taarifa za sasa



Hudhuria mafunzo kuhusu usindikaji unaozingatia viwango vya kilimo-hai ili kuboresha maanfa yako



Linda maenjo ya mazao pori na ufgajji nyuki yasichafuliwe na viambato visivyo asilia

Huu ni mwongozo wa msingi wa jinsi mkulima anavyoweza kuthibitishwa. Kwa habari zaidi wasiliana na Shirika lako la Kilimo-hai katika anuani zifuatazo:



BOAM
P.O Box 2251, Bujumbura - Burundi
Tel +25779910345
Email:sibad53@gmail.com



NOGAMU
Plot 957 Galukande Close, Off Tank Hill Road, Muyenga, P. O. Box 70071, Clock Tower, Kampala, Uganda.
Tel: +256 312 264039
admin@nogamu.org.ug
www.nogamu.org.ug



KOAN
ICIPE Complex, Kasarani Road
P.O. Box 72461-00200 Nairobi, Kenya
Tel: +254 20 2610863
Email: koansecretariat@elci.org
www.koan.co.ke



ROAM
B.P. 6886 Kigali - Rwanda
Tel +250 788558027
Email: rwandaorganicmovement@gmail.com



TOAM
Shaurimoyo/Lindi Str, Mariam Towers Bldg.
P.O. Box 70089, Dar es salaam, Tanzania
tel: +255 732 975 799
toam@kilimohai.org www.kilimohai.org



IFOAM Head Office
Phone: +49 228 92650 10
Email: headoffice@ifoam.org
www.ifoam.org



Sida
Swedish International Development
Cooperation Agency